



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA**  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KGR/BDC/S.2/70/12

08/02/2021

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kwa barua ya tarehe 28 Januari, 2021 yeye Kumb. Na. FA.170/368/01”B”/50 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hiyo, anawatangazia Watanzania wote wenye Sifa na uwezo wa kujaza nafasi **02** kama inavyoonekana hapa chini:

### **MSAIDIZI WA KUMBUKUMU II – (NAFASI 02) – TGS B**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na elimu ya kidato cha IV au cha VI.
- Awe na cheti cha Astashahada (**Technician Certificate - NTA LEVEL 5**) cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

#### **MAJUKUMU YA KAZI**

- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaii yanayohitajika na wasomaji.
- Kuthibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu,nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka kumbukummbu (barua, nyaraka nk) katika mafaii.

---


Sanduku la Posta 491 Bukoba, Kagera **Simu:**  
028 2220287, **nukushi:** 028 2221839 **barua pepe:** [ded@bukobadc.go.tz](mailto:ded@bukobadc.go.tz), **tovuti:** bukobadc.go.tz

- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

### **MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI.**

1. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
2. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa.
4. Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**Statement of Results havitakubalika**).
6. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **Wasiombe Kazi** na wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
7. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe **kwa njia ya Posta** kabla ya tarehe **23/02/2021** kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 491,  
**BUKOBA.**



Babylus Lubigo Mashauri  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA**  
**S.L.P 491**  
**BUKOBA**

Nakala kwa: Ubao wa Matangazo,  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P 299,  
**KAGERA.**

“ “ Ubao wa Matangazo,  
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,  
S.L.P 9,  
**BUKOBA.**

“ “ Ubao wa Matangazo,  
Halmashauri ya Manispaa  
**BUKOBA.**